HOTUBA YA MHESHIMIWA GAVANA JOHN OBIERO NYAGARAMA KATIKA SHEREHE ZA MASHUJAA DEI TAREHE ISHIRINI OKTOBA 2016 KATIKA ENEO LA EKERENYO

"Mabibi na mabwana,

Kwangu mimi, sherehe za kila mwaka za Mashujaa Dei zinaashiria mambo matatu. Kwanza, ni kitendo cha ukumbusho. Tunawakumbuka watu ambao hapo mwanzo, walikuwa na masuala yao ya kibinafsi. Wote walikuwa watu wenye maazimio: Kukamilisha masomo, kupata mtu wa kupenda, kuanzisha familia, kuanzisha Biashara ama kuendeleza taaluma na kuishi maisha ya amani. Lakini, walipokumbana na masuala ambayo yaliwaathiri pamoja na wananchi wenzao, walijipata katika njia panda. Walikuwa na chaguo la kutilia maanani mambo yao ya kibinafsi na kuachilia mbali yalokuwa yakiendelea lakini walichagua kutupilia mbali masuala yao ya kibinafsi. Walifahamu kwa hakika hatari zilizoambatana na kuasi waliokuwa na mamlaka lakini hawakuyumbishwa. Walijua kwamba pasi na kutumia akili na nguvu zao kupinga hayo, maovu ya dhuluma na ukatili yangeendelea bila kikomo. Hawa ndio tunaowatambua kama mashujaa. Hawa walikuwa watu wa kawaida waliowekwa katika hali ambazo sio za kawaida lakini bado wakaamua kufanya mambo yaliosawa.

Pili, sherehe hizi pia ni shukrani. Leo hii kwa sababu ya kujitolea kwao kama sadaka, tunafurahia aina mbali mbali za Uhuru: tuko huru kutokana na wavamizi; vurugu na athari za vita; sasa tuko huru kutokana na uongozi wa kiimla. Tuko huru kupeana maoni yetu na kuafikia ndoto zetu.

Jambo la tatu na ambalo ni muhimu kwangu ni kwamba, ni fursa ya kutafakari maana halisi ya kuwa shujaa, na sio tu kwa siku zilizopita bali katika hali zetu za sasa.

Mabibi na mabwana, ni muhimu kwangu kufafanua ushujaa. Sisi ni watu wa tabaka mbali mbali na uwezo wa kutofautiana. Na hivyo, kila mmoja wetu ametunukiwa nafasi ya kipekee ya kuzitumikia serikali zetu (iwe ile ya kitaifa au ya kaunti) na wakenya wenzetu.

Katika upande wetu, **Mabibi na mabwana**, serikali imeunda sera mwafaka ambazo zitatusaidia kuimarisha mafanikio ambayo tumekwisha kupata. Mikakati ya sera ambazo ziko katika bajeti ya mwaka huu inanuia kuimarisha mafanikio tulioyapata na kuboresha maisha ya watu wa Nyamira. Ndio sababu tumetenga rasilmali katika sekta za maji, miundomsingi, afya, elimu, kilimo, vijana na maswala ya kijamii ambayo pia, yatainua ukuwaji na kubuni nafasi za kazi.

Ninakariri kwa ujasiri kwamba, serikali yangu imeleta Huduma za matibabu na za bei nafuu karibu na wananchi. Tumempa kila mtoto nafasi ya kufaidika na elimu ya kimsingi na Huduma bora ya watoto. Tumefungua barabara mpya kupitia mashine zetu na kupeana kandarasi. Pia, tumeweka mikakati kupitia mfumo wa wafanyakazi ili kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapokea ujuzi ili kujiunga na nguvukazi kupitia ajira ya kibnafsi na kuwaandaa kwa ajili ya ushindani wa soko la kitaifa na kimataifa. Wakulima pia wamelindwa kutokana na mawakala walaghai na kupokea pembejeo za kilimo na huduma kwa kwa bei zilizopunguzwa.

Mabibi na mabwana,

Tumeanza tu, na tunahitaji kila mmoja wenu kutuunga mkono katika kila njia. Watu wa Nyamira wanahitaji maendeleo. Hivyo basi, tunatiwa changamoto ya kuonyesha matokeo kupitia miradi na mipangilio iliyowazi. Kwa hivi sasa, tunatathmini mikakati yetu na kuunda mipangilio muhimu ya utekelezaji. Kwa hakika, tunakabiliana na changamoto tunazokumbana nazo katika hali ya kujitolea. Ninakubaliana kwamba, kulingana na manifesto yangu, watu wa Nyamira wanahitaji maisha yaliyo na afya bora, mfumo bora wa uchukuzi, uwekezaji wa mafanikio, kilimo cha mazao bora na uchumi wenye mafanikio.

Katika hali hii, kutokana na makadirio ya fedha ya mwaka huu, mabibi na mabwana, serikali yangu inalenga kwa makini mkakati wa kaunti wa Fedha wa mwaka 2016/2017 ambao unapatia kipao mbele miradi ya idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi; Uchukuzi, Barabara na Ujenzi wa Umma; Huduma za matibabu, Maji, Mazingira, Nishati, madini na mali asili; Jinsia, Vijana, Michezo, Utamaduni na Huduma za jamii na Ardhi, Mipango na maendeleo ya mjini. Miradi hii yote iliyotambuliwa, italeta maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa upesi ambayo yatapiga jeki nafasi za utengenezaji wa mali miongoni mwa watu wetu.

Mabibi na mabwana, ni kwa sababu hii ambapo niliamrisha kila idara kutambua miradi ya maendeleo na maeneo ambayo yanafaa zaidi kwa ufadhili. Hivyo, tumependekeza kupeana fedha zaidi kwa miradi mikubwa ambayo itahakikisha kwamba kaunti yetu inapiga hatua na kupanda katika kiwango kingine cha maendeleo kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo chini ya mpango wa matumizi ya muhula wa kati.

Mabibi na mabwana, ningependa kuwahakikishia kwamba, serikali yangu iko tayari kufanya kazi bila kuchoka ili kujenga siku za usoni ambazo watu wote watajivunia na kushiriki faida kulingana na kauli ya: ***nyamiracounty#HapaNiKaziTu!***

Mabibi na mabwana, kwa miaka minne ambayo tumekuwa mamlakani, serikali yangu imeasisi sera ambazo zinainua hali ya maisha ya watu wetu. Nafurahi kusema kwamba hata kama tumekabiliana na changamoto chache, safari yetu imekuwa ya fanaka.

Mabibi na mabwana, Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wetu na mafanikio yake yatachangia katika ukuzi wa uchumi wa kaunti yetu kwa jumla. Mikakati yetu ya hapo awali imeinua mazao ya mimea na mifugo kwa kiwango kikubwa. Miradi ya nyongeza ya ubora na zaidi ya greenhouse mia nane zimeanzishwa kote katika kaunti. Hivyo, tunaendelea kuimarisha mikakati ya kuinua kiwango cha chakula, kupunguza umaskini na kuongeza mapato ya wakulima wa kiwango cha chini.

Katika sekta ya mifugo, serikali yangu imepeana huduma za upandikizaji wa mbegu au Artificial Insemination kwa zaidi ya mifugo elfu ishirini ambao wameongeza mazao yao ya maziwa kutoka lita laki sita hadi lita laki nane na elfu hamsini. Ili kupanua uafikiaji wa huduma za kilimo, tumenunua vipoza maziwa, kusambaza miche ya ndizi aina ya tissue culture na kupeana samaki wadogo wa kufuga kwa wakulima wetu.

Kwa ushirikiano na Chuo kikuuu cha Kilimo na Teknolojia cha Jomo Kenyatta (JKUAT) **mabibi na mabwana**, tumetenga shilingi milioni thelathini kwa ujenzi wa mahabara ya bioteknolojia ili kuisaidia kaunti yetu kuzalisha ndizi aina ya tissue

culture kwa kiwango kikubwa na kuongeza mapaato kupitia uuzaji wa miche katika eneo hili. Hii, kwa hakika itapunguza gharama ya uzalishaji na kubuni nafasi za kazi kwa watu wetu.

2. Huduma bora za afya kwa wote

Mabibi na mabwana, serikali yangu imefanya mabadiliko makubwa katika huduma za afya kwa kuasisi njia bunifu za kuimarisha kiwango cha huduma hizi huku zikipunguza gharama yake. Huduma za afya ni kipengele muhimu katika bajeti yetu na hupata jumla ya mgao wa zaidi ya robo ya fedha zote. Hadi sasa, tumeimarisha kiwango cha vifaa vya matibabu, wafanyakazi na huduma nyinginezo za afya. Serikali yangu inafanya kila juhudi ili kuimarisha mfumo wetu wa afya ili kuafikia viwango vya Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO). Kuondoa vifo vywa watoto wachanga ni swala ambalo tumelipa kipau mbele na ndiposa, tumewekeza katika huduma za uzazi zenye sheria kali. Umbali hadi vituo vya afya pia umepungua. Aidha, ningependa kusema kwamba mapato yanayotokana na vituo vyetu vya afya yameongezeka kwa kiwango kikubwa.

Suala la kutokuwepo kwa madawa katika vituo vyetu vya afya limezikwa katika kaburi la sahau. La muhimu zaidi, **mabibi na mabwana**, sasa unaweza kupata huduma za afya kwa urahisi.

Mabibi na mabwana, ili kuhakikisha kwamba tuna mfumo na mazingira yanayopiga jeki utekelezaji wa huduma za afya za uzuiaji kupitia uchunguzi, uimarishaji wa afya tiba na huduma za kurekebisha, serikali yangu;

i. Itajenga wadi yenye vitanda themanini ikiwa pamoja na sehemu ya madaktari katika Hospitali ya Rufaa ya Kaunti ya Nyamira na kununua vifaa vya kimatibabu vya hali ya juu kwa matumizi humo.
ii. Itaimarisha kituo cha afya cha Amatierio hadi daraja la tatu ili kupeana huduma kwa chuo kikuu cha Kiabonyoru na jamii katika eneo hilo.
iii. Itakamilisha ujenzi wa kituo cha afya cha Magwagwa cha daraja la tatu.

3. Uhifadhi wa Mazingira, upatikanaji wa maji na usafi ulioimarika

Mabibi na mabwana, ushahidi wa fanaka katika sekta ya maji ni dhahiri katika upatikanaji wa maji katika kaunti nzima. Familia zinazopata maji safi kwa matumizi zimeongezeka. Tutaendelea kukarabati na kujenga vianzo vya maji kuhakikisha kuwa tunakidhi mahitaji ya maji ya watu wetu. Ni wazi kwamba, uamuzi wetu wa kuwapa watu wetu maji safi umepunguza kuenea kwa magonjwa yanayotokana na maji chafu. Ili kuhakikisha kwamba watu wetu wanapata maji safi na ya kutosha, serikali yangu imetenga fedha za kufadhili lengo hili. Ili kushughulikia maji taka, serikali imeweka mikakati ya ukarabati na uhifadhi wa maeneo ya mjini na mali asili.

Kando na hayo, tutaendelea kupiga jeki uchumi wa kijani kibichi kwa kuongeza kawi ya miyale ya jua ya kuleta mwangaza katika barabara. Kwa wale ambao hawajiwezi katika jamii na ambao hawawezi kupata nguvu za umeme serikali yangu itawanunulia vifaa vya kuleta mwangaza kwa kutumia miyale ya jua ili wapate mwangaza. Kwa sababu ya kuleta mwangaza katika barabara zetu, usalama umeimarika na masaa ya kufanya Biashara kuongezeka hadi saa mbili za usiku. Hata hivyo, mpango huu umepata changamoto ya kuporwa na wahalifu wachache ambao serikali yangu itahakikisha kwamba wanatiwa nguvuni na kushtakiwa kulingana na sheria.

4. Kuimarisha Elimu na sekta ya Vijana

Mabibi na mabwana, katika muda wa miaka mitatu iliyopita, tumeshuhudia ongezeko kubwa la usajili katika vituo vya elimu ya kimsingi yaani ECDE. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba kila mtoto katika sehemu za mashambani anapata elimu katika umri unaofaa. Kwa sababu hii, **Mabibi na mabwana**, walimu mia nane na kumi na watano wameajiriwa kuhudumia watoto waliosajiliwa katika vituo vya elimu ya kimsingi. Serikali yangu kwa jumla imejenga vituo vya elimu ya kimsingi na kuvipatia madawati na vifaa vingine vya masomo. Taswira ya madarasa mabovu ya udongo na mbao sasa inatoweka pole pole lakini kwa njia ya ustadi.

Pia, tumewekeza katika ujenzi wa vyuo vya kiufundi ishirini na sita ili kukuza ujuzi wa vijana wetu katika harakati za kuwatayarisha kuwa mahiri katika ajira. Na jinsi ambavyo nimekuwa nikisema kila mara, tunahitaji waashi, wataalamu wa vyuma, wahandisi wa nguvu za umeme na mekaniki, wasorovea wa upimaji wa wingi,

wataalamu wa ujenzi wa miji na wengi wengine na tutazidi kuwekeza katika ujenzi na urekebishaji wa vyuo vyetu vya kiufundi.

Mabibi na mabwana, ni furaha yangu kusema kwamba, karakana zote katika kila chuo cha kiufundi kimekarabatiwa nakupewa vifaa vya masomo. Usajili wa wanafunzi katika vyuo hivi pia umeiongezeka pakubwa. Ninaamini kwamba tunaendelea kujitahidi ili kuafikia kuwa kitovu cha wanadamu wenye ujuzi katika siku za usoni. Serikali yangu itaendelea kununulia vyuo hivi vya kiufundi vifaa vya masomo. Aidha, tayari tumekamilisha ujenzi wa karakana ishirini na sita katika vyuo vya kiufundi na kuajiri wakufunzi wenye ujuzi. Tena, tutajenga vituo ishirini zaidi vya elimu ya kimsingi yaani ECDE.

Mabibi na mabwana, hivi majuzi tulizindua mpango wa ajira ya vijana wa kijamii ili kusaidia katika usimamizi wa barabara, usafishaji wa masoko, usalama na uhifadhi maeneo ya kutega maji na upanzi wa miti katika kaunti yetu kupitia kwa vijana. Jumla ya vijana thelathini na tano kutoka kila wadi walihusishwa katika mpango huu.

Kupitia kwa mikakati kama hii **Mabibi na mabwana**, tunapanga kupunguza ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana wetu. Vijana watahitajika kuunda vikundi ambavyo vitawawezesha kupata mikopo ili kujiimarisha kiuchumi kupitia kwa mpango wa kitita cha Nyamira Youth Empowerment Fund na hatimaye, kuanzisha kuzalisha mali.

5. Kufadhili maendeleo ya miundo msingi

Mabibi na mabwana, miundomsingi iliyoimarika ni kiungo muhimu katika maendeleo endelevu ya kiuchumi kwa sababu ya uhusiano iliyonayo na sekta zingine za uchumi. Katika hili basi, sekta hii imewekeza rasilmali katika upanuzi wa mtandao wa barabara, kukarabati barabara zilizopo na uhifadhi wa vituo vya miundomsingi.

Ninakiri kwamba, serikali yangu imepiga hatua kubwa za kushabikiwa katika kufungua barabara ili kuimarisha mtandao wa uchukuzi licha ya sisi kuwa na rasilmali finye. Mpango maarufu wa MTF ambao mimi mwenyewe ninauangalia katika kila wadi ulikuja kwa wakati unaofaa. Matokeo yake ni ya kutia moyo na muda si muda, kaunti yetu yote itakuwa na barabara zinazopitika kwa urahisi kwa

uchukuzi na Biashara. Kwa kunakili, tumefungua kilomita mia mbili za barabara mpya na kilomita mia nne za barabara. Haya ni maendeleo makubwa. Tumeanza tu. Nina hakika kwamba maendeleo ya miundomsingi haswa mfumo wa barabara yatakuwa sehemu kubwa ya urithi wangu baada ya kumaliza muhula wangu kama Gavana mwanzilishi wa kaunti hii kubwa ya uwezekano.

Mabibi na mabwana,

Uwekezaji na Biashara ni vigezo muhimu katika ukuaji wa uchumi kutokana na ewezo wao wa kuleta mali na kubuni nafasi za kazi. Ili kuimarisha biashara katika kaunti yetu, tumejenga masoko mapya kuchukua nafasi ya yale yaliokuwepo mabovu na yenye usimamizi mmbaya kabla ya sisi kuingia mamlakani. Tunaamini kwamba biashara inayoshamiri inaweza kuinua kiwango cha maisha kwa maelfu ya watu. Hii ni kumaanisha kwamba, mfanyabiashara anaweza kuishi katika Nyumba bora, kuwalipia karo watoto wake, kukidhi mahitaji ya familia yake, kupata huduma bora za kiafya na kufanya uwekezaji.

Ili kuhakikisha kuwa waendeshaji pikipiki wanapata urahisi katika kufanya shughuli zao kupitia eneo maalum la uthibiti, **mabibi na mabwana**, tumepanga kujenga vituo vya Bodaboda katika kila wadi. Zaidi ya hayo, mwaka huu tutajenga kituo kimoja cha bodaboda katika kila lokesheni ya utawala wa Mikoa. Katika ruwaza ya **"Nyamira tuitakayo ya mwaka 2020",** tunapania kujenga vituo vya bodaboda katika kila soko. Pia, tunafanya mazungumzo na washika dau wengine ili kutoa mafunzo ya usalama barabarani kwa waendeshaji hawa na kuwasaidia kuunda makundi ya kibiashara.

Pia, tunajenga eneo la kuegesha magari katika mji wa Nyamira na kufufua ujenzi kwenye maeneo ya watu kutembea katika jitihada za kupunguza msongamano wa magari katika barabara kuu. Sehemu ya maegesho kati ya benki ya Equity na ofisi za idara ya ujenzi wa umma imeinua hadhi ya mji wetu wa Nyamira na bila shaka tutapokea mapato bora kutokana na ada ya maegesho.

Mabibi na mabwana,

Serikali yangu imeasisi mikakati ya mabadiliko katika Vyama vya Ushirika ili kuimarisha kilimo na sekta ya Jua Kali. Hivi Vyama vya Ushirika vinaajiri watu wengi kando na kutoa nafasi za ajira ya kibinafsi na mengine mengi. Na kwa sababu

hii, Mabibi na mabwana, tunawekeza rasilmali nyingi katika ukuwaji wa vyama hivi na kuhakikisha usimamizi bora wa kibiashara katika vyama vya hivi na Biashara ndogo ndogo. Aidha, tumetenga fedha zingine kwa ajili ya kupeana mikopo ya bei nafuu na kuimarisha ujuzi wa kibiashara.

8. Ulinzi wa kijamii kwa makundi ya wasiojiweza

Mabibi na mabwana,

Kama serikali inayoshughulikia masuala ya wanyonge katika jamii, tumetenga fedha za kufadhili makundi kama vile ya walemavu na wazee mradi tu wasiwe wanapokea misaada kutoka kwa serikali ya kitaifa.

9. Kukuza Talanta

Mabibi na mabwana,

Serikali yangu iko makinifu katika kukuza na kuwekeza katika talanta za vijana wetu. Talanta ambayo imekuzwa vema ni ya manufaa makubwa kwa jamii. Ili kukuza talanta, tunapendekeza katika bajeti ya mwaka huu kutenga fedha tosha katika ununuzi wa vifaa vya kuimarisha vituo vyetu vya talanta.

Serikali yangu inaendeleza ujenzi wa viwanja vya michezo vya Manga na Nyamaiya ambavyo vitasaidia katika michezo mbali mbali. Kwa kuwa uwanja wa Nyamaiya umetambuliwa na kupitishwa kuwa uwanja wa maonyesho ya kilimo, tumekusanya fedha za kuinua hadhi yake ili kukiwezesha kuafikia malengo yake. Wakati huo huo, tumefanya mipango ya kuimarisha viwanja vya michezo vya Ekerenyo, Esigere, Sironga, Nyansiongo, Rigoma na vile vya shule za umma katika kaunti yetu. Yote haya, ni kwa ajili ya kuimarisha michezo katika kaunti yetu.

Mabibi na mabwana,

Hatua hizi hizi zimeafikiwa kutokana na jitihada za maafisa wangu na mikakati mwafaka. Uungwaji mkono wa wananchi kupitia hafla na mipango za ushirikishi pia, zimechangia pakubwa. Kupitia mpango wetu wa kila juma wa Gavana Mashinani pamoja na majarida ya idara, miingilio yetu imechochea mitazamo na shughuli zetu kuhusu matarajio ya wananchi kutoka kwa serikali yangu. Tunaitikia zaidi yale mambo mnayotaka sisi kuwatendea kuliko yale tumeyatengeneza kwa ajili yenu. Na kwa hakika, huu ndio ugatuzi ambao kwa kiasi kikubwa ni demokrasia katika ushirikishi

wa umma inavyosheheniwa katika katiba yetu. Uhalali wa chochote tunachokitenda umesheheniwa katika kuhusishwa kwenu na hivyo, ninawasihi kutenga muda ili kuungana nasi katika kupiga jeki mikakati yetu ya maendeleo. Aidha, ninawasihi kwamba tunapokuwa na hafla za ushirikishi wenu, muwe watu wastaarabu na wenye mawazo sawa haswa mnapotueleza yale mnayoyatarajia kutoka kwetu kama serikali.
Kwa ajili ya ushirikishi wa kufana, serikali yangu imeanzisha kitengo cha Ushirikishi wa Umma na Elimu ya Uraia na kuweka mifumo, wafanyakazi na mambo muhimu katika ufanisi wake.
Ninawahakikishia ya kwamba, serikali yangu inafanya kazi katika nyakati na malengo yaliyowekwa na hivyo, maafisa wangu hawafanyi kazi kiholelaholela. Hii ni kwa sababu serikali yangu inazingatia utiaji sahii wa kandarasi za utendakazi na mfumo wa kuwapiga msasa wafanyakazi katika kaunti tangia mwaka wa 2013. Matokeo ya mifumo hii katika serikali yetu kupitia kwa sera ya mfumo wa utendakazi na uwajibikaji wa mwaka 2014 yamedhihirika katika sekta zote. Na mwaka huu, haujaachwa nje. Juma lililopita, siku ya jumatano, niliwaongoza mawaziri wangu ili kutia sahii kandarasi za utendakazi kulingana na malengo ya idara zao ambayo ninatarajia waafikie bila kisingizio. Hapana njia ya mkato. Ni lazima watu wetu wapate huduma bora na kwa wakati ufaao bila ya upungufu wa kutoafikia malengo yetu.

Katika tamati, Mabibi na mabwana, nyinyo nyote ni mashujaa katika haki zenu. Nyinyi ndio wale mashujaa wengi ambao hawajatambulika- ambao vitendo vyao havijulikani na wengi. Wakenya ambao hawakati tamaa wanapokumbana na dhiki, waliosaidia na kufanya kazi na wananchi wenzao bila kusita. Wapo walimu wengi wanaojitolea kuelekeza vizazi katika njia za mafanikio. Wapo wanchi wengi wanaoheshimu sheria ambao huchagua kuyatekeleza majukumu yao pasi na kuingia majaribuni ya kupata pesa za haraka.

Wapo askari wetu ambao wanalinda mipaka yetu na watu wetu kwa ujasiri wa kweli. Wapo wanataaluma wanaotumia ujuzi na elimu yao kuwahudumia wakenya wenzao. Ni viongozi wa taasisi za kidini ambao ni marafiki wetu katika kupigana vita dhidi ya ufisadi na kupiga jeki mageuzi humu nchini. Wapo pia wananchi mbali mbali wenye utu wema wanaofanya juhudi na kuafikia mafanikio ili kuwa wenye manufaa katika jamii. Kwa niaba ya serikali ya kaunti ya Nyamira,

ninawashukuru nyote. Nyinyi haswa, ni thibitisho kwamba jamii yetu ni kitovu cha mashujaa.

Mabibi na mabwana, hapa karibu katika kaunti ya Nyamira, tumekuwa tukitembea katika njia nyoofu kwa miaka minne sasa. Mbegu za mabadiliko ambazo tumepanda tayari zimeanza kuzaa matunda na tunavyoona, wale wanaotaka kuwatumia vibaya watu wetu, wamekata tamaa. Tusije tukapoteza nafasi tuliyonayo leo. Hii ndio njia ya pekee ambayo kwayo tunaweza kuwalipa na kuwaheshimu mashujaa waliojitolea kwa mno kama sadaka ili taifa letu liweze kufika mahali limefika leo. Hii, ndio njia ya pekee ya kuhakikisha kuwa vizazi vijavyo vinapoadhimisha Mashujaa Dei, vinaweza kukumbuka, kushukuru na kutafakari sura hii ya historia yetu na waseme: hakika huu ndio wakati wakenya wote kwa jumla, haswa watu wa Nyamira, waliamua kama watu wa jamii moja kuwa mashujaa.

Asanteni na Mungu awabariki.”